**DIBAJI**

Ndugu Joas Yunus Buyungu ni mwandishi kijana mwenye uzoefu mkubwa na masuala ya habari za kimitandao. Binafsi nimemfahamu Joas kuwa ni mtu mwenye wivu mkubwa katika kumtumikia Mungu, ana uwezo mkubwa kuhamasisha vijana na kanisa kwa ujumla kutumia mitandao kufikisha ujumbe wa neno la Mungu kwa kutumia njia za kisasa.

Ameandika kitabu hiki ili kulihamasisha kanisa na waamini wake kuamka na kufumbua macho ili kuitumia teknolojia hii ambayo huwakutanisha maelfu ya watu ulimwenguni kote. Kitabu kimeandikwa kwa lugha rahisi ambayo mshirika yeyote anaweza kuelewa na kuanza kutumia njia hizo bila kuwa na elimu kubwa ya Teknolojia ya habari(IT).

Lengo kubwa la mwandishi ni kuhakikisha kanisa linaendana na mabadiliko ya nyakati na mbinu katika kutimiza angizo kuu la Bwana wetu Yesu Kristo linalopatikana katika Mathayo 28:19 – 20.  Kanisa limeagizwa kuwafanya watu wanafunzi na kufundisha kweli yote ya Yesu. Kazi hii ni kubwa na nzito, inahitaji rasilimali watu, fedha na muda. Ukizingatia maneno ya Bwana Yesu mwenyewe pale alipowatuma wanafunzi wake wawili wawili kwenda kuhubiri injili utagundua kuwa hitaji la watendakazi ni kubwa kuliko tunavyoweza kufikiri. Yesu anasema mavuno ni mengi watenda kazi ni wachache (Lk.10:2); tena akasema "…inueni macho yenu myatazame mashamba, yakuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno" (Yn. 4:35). Hii inayonyesha kuwa kazi ni kubwa tena yenye udharura kiasi kwamba inahitajika kufanyika sasa.

Yesu hajataja mbinu ambazo tutazitumia wakati wote kwa vizazi vyote. Yeye alizunguka huko na huko akihubiri hadharani na manyumbani, katika maziwa na visima katika nchi ya Palestina. Paulo akatumia mbinu ya kusafiri na kuvuka mipaka ya kimataifa hadi Asia ndogo akikutana na watu mbalimbali wakiwemo wafalme na wasomi kwenye maeneo ya kumbi, masinagogi, viwanja vya riadha vya kiyunani na akaongeza mbinu mpya ya kuwasilisha ujumbe kwa barua (nyaraka za Agano Jipya). Kwa mifano hiyo ya Yesu na Paulo tunaweza kusema kwa usahihi kabisa kuwa mbinu za kutekeleza agizo kuu zinabadilika kutoka kizazi hadi kizazi.

Kitabu hiki kinaonesha kuwa kwa wakati wetu mbinu za kuwasilisha ujumbe zimebadilika kabisa ukilinganisha na za Yesu, Paulo na mitume wengine. Leo hii watu wanawasiliana kwa teknolojia ya habari zikiwemo barua pepe (email), facebook, WhatSapp, Youtube, na zingine nyingi. Dunia imehamia huko na kanisa linapaswa kuhamia katika ulimwengu

huo wa mitandao ya kijamii ikiwa linataka kubakia katika kuihudumia jamii inayoizunguka.

Kwa mtazamo wa mwandishi ni kuwa sote tunahusika na Agizo Kuu, kanisa na waamini moja kwa moja tukitumia njia hii kuwasilisha ujumbe wa uzima, tutawafikia watu ambao sio rahisi kuwafikia hata kama tutatuma wamisionari waende huko. Fikiria nchi ambazo ambazo hurusiwi kusema neno la Kristo wazi wazi, utafikaje huko hata kama ungependa, fikiria gharama za kumsafirisha na mkutunza mishenari moja tu na familia yake. Njia hii ya kutuma mishenari bado inafaa katika kutimiza Agizo Kuu, lakini lazima kuwe na njia nyingine rahisi na isiyo na gharama kubwa, hiyo ni njia ya kutumia mitandao ya kijamii. Ni matumaini yangu kuwa kitabu hiki kitakuwa baraka kwa wasomaji.

Mch. John Tuu



Mkuu wa chuo cha Biblia Sanjaranda
Mkuu wa Idara yaTheolojia (FPCT)